# Rebeka, Mwanamageuzi wa Kimaasai




Mwandishi: Olivia Wood
Mchoraji: Renson Kole
Tafsiri: Mourice Wabwire

ASHOKA
Worldreader


Rebeka, Mwanamageuzi wa Kimaasai ni hadithi ambayo imechochewa na kisa halisi cha maisha ya msichana mdogo kutoka taifa la Kenya aliyechochewa na mabadiliko ya hali ya anga katika jamii yake. Alijifanyia utafiti kuhusu suala hilo, kisha kuwalazimu wanakijiji na serikali kuchukua hatua mwafaka.

Kitabu hiki cha picha kwa watoto ni tukio la ushirikiano kati ya Ashoka na shirika lisilo la kiserikali la Worldreader. Kimelenga kuwahimiza watoto wote kuwa watu wa kuleta mageuzi na kuwahimiza watu wazima kuwaunga mikono katika safari hiyo.

Katika kijiji cha jamii ya Kimaasai, Kusini-magharibi mwa Kenya, kuna msichana anayejulikana kama Rebeka.

Rebeka anaishi karibu na mbuga kubwa sana ya wanyama, mahali ambapo pana wanyama wa kipekee kama vile simba na ndovu wakubwa wa kijivu.

Familia ya Rebeka inawafuga ng’ombe, kondoo na mbuzi na inategemea kilimo cha shamba kwa minajili kupata chakula cha mifugo wao. Rebeka huenda shuleni na pia huisaidia familia yake kutunza mifugo wakati ambapo yupo nyumbani.



Wakati wa kiangazi, mimea na wanyama hukosa maji. Siku hiyo yenye joto kali Rebeka alimpata mama yake akilia.


“Mimea yetu haijafanya vizuri mwaka huu,” alilalama mama. “Sasa mbuzi na kondoo wetu watakufa.”



Shuleni, Rebeka anamuuliza mwalimu wake mbona kumenyesha mvua kidogo tu mwaka huu?

“Tumekuwa na siku nyingi bila ya mvua,” alisema mwalimu wake. “Tunapokosa mvua mimea hunyauka na haiwezi mea tena. Bila ya mimea ya kula, maji ya kunywa , mifugo wetu hufa.”

Kila mmoja alikuwa kimya mle darsani. Walikuwa wakihofia familia zao, mifugo wao na jamii yao kwa ujumla.



Katika maktaba ya shule, Rebeka anafanya utafiti kuhusu mvua.

Matokeo ya utafiti wake yanamshangaza. Dunia nzima inaendelea kuwa na joto la hali ya juu. Rebeka anakumbana na msamiati mpya: “Mabadiliko ya hali ya anga.”

Magari madogo, mabasi na ndege yanachafua hewa. Ukataji wa miti inayotumika katika ujenzi. Pia uzikaji wa taka ardhini, vitu hivi vyote vinachangia katika uharibifu wa mazingira.



Kwa siku nzima sasa, Rebeka bado ni mwenye huzuni. Ni nini ambacho msichana mmoja anawezakufanya ili kuisaidia dunia nzima?

Rebeka anaamua kujadiliana na mwalimu wake kuhusu alichokisoma kwenye maktaba. “Ni tatizo kubwa sana kwa dunia,” mwalimu wake alieleza. “Bali kuna vitu ambavyo tunawezakufanya ili kusaidia, kwa mfano upandaji miti ili kuimarisha asili.”



Rebeka anaporejea nyumbani kutoka shuleni, kiwango cha joto kiko juu, anasimama kunywa maji kutoka kwa chupa yake. Anasongwa na mawazo juu ya ukosefu wa mvua na jinsi ambavyo anaweza kusaidia jamii yake.


Pindi likamjia wazo. “Nimejifunza mengi sana kuhusu mabadiliko ya hali ya anga,” alifikiria. “Ingesaidia sana iwapo kila mmoja angefahamu changamoto hii!”



Siku iliyofuata Rebeka alimuomba mwalimu wake kufunza kuhusu mabadiliko ya hali ya anga duniani na uharibifu unaofanywa na binadamu kwa maliasili.

Baada ya kukamilika kwa somo, Rebeka alisimama. Alimuomba kila mmoja darasani kwenda nyumbani na kuwafunza wazazi kuhusu yale ambayo walikuwa wamejifunza siku hiyo.

Baada tu ya siku chache tu, kila mmoja alikuwa akizungumzia jinsi ambavyo wanadamu walikuwa wakidhuru asili ya kilimwengu.



Siku moja wazee kijiji waliandaa mkutano na Rebeka kujadili kuhusu nini kinachoweza kufanywa ili kunusuru asili ya ulimwengu. Shuka zao ni za rangi nyekundu na wamevalia shanga vichwani na mikononi mwao.

Changamoto wanazokumbana nazo ni kubwa sana. Wingi wa uchafuzi wa mazingira hutokea katika miji mikuu, mbali na jamii yao.

“Wacha tuandike barua kwa rais wa Kenya,” Mzee kijiji mmoja alisema. ‘’ Anapaswa kujua kuwa hatuwezi kuishi bila ya mvua. Pia labda ataweza kufanyia marekebisho sheria zetu ili kuzuia uharibifu wa mazingira.”



**2** Shuka ni kitambaa cha rangi rangi kinachovaliwa na Wamaasai

Rebeka alichukua barua na kuwashirikisha wanafunzi wenzake. Wote waliwaomba wazazi wao kutia sahihi pale chini kuonyesha uungaji mkono wa suala hilo.



Jijini Nairobi, Rais anasoma barua ile kutoka jamii ya Kimaasai. Pia amewezakumbana na barua nyingine nyingi kutoka pande tofauti tofauti za nchi. “Ninahitaji kuwasaidia Wakenya kutunza mazingira,” alifikiria.


Katika jamii ya Kimaasai, kila mmoja anakubali kupanda miti nje ya nyumba zao. Rebeka na mama yake wanachimba shimo pamoja ili waweke mche mchangani.



Katika shule anakosomea Rebeka, mwalimu mkuu anazungumza na wanafunzi wote. Wanamuomba Rebeka kusonga mbele.

“Kutunza mazingira ni kazi kubwa sana na kila mmoja duniani anapaswa kusaidia.” Mwalimu mkuu alisema, “Bali tungependa kutoa shukrani haswa kwa kutusaidia kufahamu kuleta madiliko. Hebu fikirini iwapo sisi sote tungeweza kusaidia jamii yetu!’’

Rebeka alikuwa mwenye furaha sana. Alikuwa tayari anafikiria kile ambacho yeye na rafiki zake wangeweza kufanya tena ili kutunza mazingira na kusaidia jamii yake.



**Tukio #1**: Mpende jirani
**Kundi la umri:** 3-8
**Ujuzi:** Huruma, Mawasiliano
**Nyenzo:** Viti
**Mbona?** Ili tuweze kutatua tatizo, tunapaswa kuelewa tajriba za watu wengine na uelewa wa changamoto tofauti tofauti. Lazima tuwe na zaidi ya mtazamo wa kwanza na maandiko ya kijuujuu tu na kubadilisha miradi yetu na matarajio na ufahamu. Ni muhimu sana sisi kuwa na uhusiano mwema na wanadamu wenzetu na kuhisi kudhaminiwa.

**Vipi?** Mchezo ufuatao ni mzuri katika kubaini tajriba sawia miongoni mwa wanafunzi. Kwa kuchochea ufahamu wa kihistoria na mapendeleo yao na kuhamasisha uanajamii. Mchezo unawezafanyika darasani ama nyumbani.

**1. Maandalizi:** Kabla ya kuanza mchezo, tayarisha viti vikilingana katika mduara. Waeleze wahusika kuwa kila mmoja atapata nafasi na hakuna haja ya kuvikimbilia viti. Wakaribishe wote kwenye viti waketi katika mduara.

**2. Mchezo:** Mchezo unaanza pale ambapo mhusika mteule anasimama katikati ya mduara na kusema habari za kweli kumhusu. Kwa mfano, “Ninampenda jirani yangu aliye na ndugu mdogo.” Kila mmoja ambaye ameketi na habari hizi ni za kweli ni sharti asimame na kusongesha kiti chake kando, kisiwe mkabala na mtu huyo. Mhusika aliye katikati ya mduara pia yuko katika harakati ya kutafuta kiti na hivyo kumwacha mhusika mmoja bila kiti.
Mhusika huyo aliyekosa kiti anaingia katikati ya mduara na kuendeleza mchezo kwa kusema habari ambazo ni za kweli kumhusu. Kwa mfano, “Nampenda jirani ambaye anazungumza Kihispania” ama, “Ninampenda jirani anayependa kucheza soka.”

Mchezo unaendelea hadi kila mmoja anapata fursa ya kutoa ujumbe kumhusu.

**3. Tafakari:** Jadili kuhusu tajriba yako katika mchezo.

- Je, ulijifunza nini kutoka kwa watu wengine?
- Je, ulishitushwa na jinsi ambavyo watu walikuwa wakiruka ruka juu kwa furaha?
- Je, ulihisi vipi ulipokuwa pale katikati pekee yako?
- Je, ulihisi vipi ulipogundua kuwa watu wengine walikuwa na tajriba kama yako?

**Tukio #2:** Matumaini Yamenizunguka

**Kundi la umri:** 5-12

**Ujuzi:** Ujasiri utu na Ufahamu

**Nyenzo:** Karatasi na penseli ama kamera

**Mbona?** Mara nyingi tunakosa kuvidhamini vitu vidogo vidogo ambavyo vinatuzunguka na kuyapa maisha maana. Watu wenye mageuzi hawatambui tu changamoto bali pia hulenga fursa inayoibuka. Wanamageuzi huongozwa na matumaini bali si uoga na hasira.

**Vipi?** Katika zoezi la juma hili, vitafute vitu vitano ambavyo hukupa furaha kila siku. Kwa kufanya hivi, utaanza kuona vitu vyenye uwezo mkubwa vinavyokuzunguka pamoja na ule uwezo ulio ndani mwako.

Kila siku andika, chora ama piga picha kitu ambacho hukufurahisha. Tafakari kuhusu kile kinachofanya utabasamu na je, iwapo kinaleta tabasamu kwa watu wengine pia? Mbona unafurahia?
**Kwa mfano:** Kila Ijumaa wewe na rafiki zako huchukua vitafunio mkielekea nyumbani. Ni jambo la furaha sana kuwaona rafiki zako wakiburudikia vitafunio. Piga picha za rafiki zako na na vitafunio vyao.

**Tafakari ya mwisho wa juma**

Zungumza na rafiki yako ama mwanafamilia. Jadiliana nao kuhusu vyote vilivyokufurahisha! Je, ulijifunza nini kuhusu wewe binafsi na jamii yako?

**Tukio #3:** Hisi, Fikiria, Tenda, Shiriki

**Kundi la umri: 5-15**

**Ujuzi:** Kufikiri kwa kina, Suluhisho

**Nyenzo:** Karatasi na penseli

**Mbona?** Uelewa unaweza kupatizwa kupitia kutazama na kutafakari. Kwa mfano, kunakili kazi za ziada kunaweza saidia vijana kuyafahamu vizuri yale waliyojifunza. Maswali yenye hisia yaweza kuwasaidia vijana kuwasilisha hisia zao na wengine. Tukitafakari kuwa dunia nzuri yaweza kuwasaidia vijana kufikiria zaidi ya wao binafsi. Hili zoezi laeza fanywa kibinafsi ama katika kundi.

**Vipi?**

.

**Hatua 1:** Anza na kutathmini changamoto unayopania kuisuluhisha. Nakili hali na tabia ambazo hukuudhi ukiwa nyumbani, shuleni au katika jamii.

Baada ya kunakili changamoto hizo jiulize maswali yafuatayo: Shida ni nini? Shida hizo zina muundo upi? Je shida hizi hukufanya uhisi vipi? Je, shida hizi hawafanya watu wengine wahisi vipi?
Rudia zoezi hili kwa juma moja.

**Hatua 2: Fikiria.** Hii ni awamu ya kutoa maoni. Kulingana yale ambayo umetazama, tafakari kuhusu jinsi ambavyo changamoto huathiri wenzako.

**Jadili**: Je kina nani uliwaona kama wahusika wa tukio hilo? Je, kitu kipi kilikuwa tofauti sana kulingana na wewe? Kwa nini?

Sasa ni wakati wa chemsha bongo kuhusu suluhisho. Unahimizwa kunakili maoni mengi iwezekanavyo na hakuna kuhukumu maoni ya wengine.

**Majadiliano**: Je, tunweza kutatua tatizo hili vipi? Ni nini kipi tofauti tunawezakifanya? Je, ni njia zipi tofauti tunwezakujumuisha na maoni tofauti ili kuifanya bora zaidi?

**Hatua 3: Tenda.** Rejelea maoni yako yote. Pigia mstari maoni yale yanayokupendeza. Maoni yapi yanakufurahisha zaidi?


Sasa upo tayari kuchukua hatua. Hapa unalenga maoni na malengo ambayo ni rahisi kutekelezeka bali si yale yaliyokamilika zaidi. Jaribu kutekeleza maoni yako kichwani ukimrejelea mtumizi bali si bidhaa.

Hebu tafakari kuhusu haya;

1) Je, inafanana vipi?
2) Je, inahisi vipi?
3) Je, inatenda kazi vipi?

**Hatua 4: Shiriki.** Jadili na mtu mwingine suluhisho lako kuhusu changamoto. Pata maoni yao kwa kile kinachoweza kutekelezeka, kile ambacho hakiwezi kutekelezwa na jinsi ambayo kinaweza kuimarishwa. Wape changamoto ya kuibuka na maoni mapya pia!

## Mjue Rebeka



Rebeka ni mwanamapinduzi kutoka Kenya anayewahimiza wanafunzi wenzake kutoka shule ya wasichana na ya kibinafsi ya  Tembea na wanajamii kuwa wanaharakati wa mazingira kupitia elimu na uanaharakati. Rebeka na wanafunzi wanzake wako na jukumu la kutunza mazingira na hatua za kimsingi ni kama vile kuandika barua ya malalamishi kwa afisi za serikali.

Shule anakosomea Rebeka ilianzishwa chini ya Mradi wa BEADS for Education ,shirika lisilo la kibiashara linalolenga kuimarisha elimu ya mtoto wa kike na biashara.
Wadhamini wa Rebeka, Cynthia Moss; mwanzilishi wa Amboseli Trust for Elephants, humuhimiza sana  Rebeka kuwa mtu mwenye huruma kwa kiumbe chochote kile.
Kwa kujitolea ili kuboresha dunia, Rebeka anasema, “Nikifaulu katika malengo yangu, dunia itakuwa mahala pa kupendeza sana. Ng’ombe watanenepa, watoto watang’aa, miti itakuwa mingi, masokoo yatajaa vyakula vya shamba na hata pia wanyamapori watakuwa kwa wingi.”

## Kuhusu Ashoka

Ashoka anaamini katika uwezo wa kufanya mabadiliko na kila mmoja kufungamana na ulimwengu huu unaobadilika. Ashoka analenga kujenga jamii ya kilimwengu yenye msingi wa kila mmoja kuwa na mtazamo wa kimabadiliko. Katika akili za kila mwenye mabadiliko, vuguvugu za uanaharakati zinalenga kubadili jinsi ambavyo watoto na vijana wanakua kiasi cha kila mmoja kuwa na ujuzi wa kuleta mabadiliko kote.

www.ashoka.org

## Kuhusu Worldreader

Worldreader wanaamini kuwa wasomi huanda dunia nzuri. Tunafanya kazi na washikadau dunia kote ili kuwasaidia watu wenye mahitaji na usomi wa kidijitali na imarisha kusoma na kuandika miongoni mwa watoto.

www.worldreader.org

2021 Ashoka na Worldreader

Kazi hii ina Kibali cha Creative Commons Attribution-NonCommercial 4.0 International License.

Kwa ujumbe zaidi, wasiliana na **privacy@ashoka.org** ama **publishing@worldreader.org**